# THBUB yataka hatua kukabili ukiukwaji haki za binadamu

**NA SAIDA ISSA, DODOMA**

TUME ya Haki za Binadamu na Utawala bora tanzania (THBUB) limelaani kuwepo kwa matukio yanayoashiria uvunjifu wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora na kuzitaka mamlaka husika kuchukua hatua.

Akizungumza na wanahabari jijini Dodoma mwishoni mwa wiki illiyopita, Mwenyekiti wa Tume hiyo, Jaji Mstaafu Mathew Mwaimu, alitaja matukio hayo kuwa ni pamoja na la kushambuliwa kwa Katibu Mkuu wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Padri Dk. Charles Kitima na kutekwa kwa wanachama wa CHADEMA, Faluka Saidi Nyagali 'Mdude' yaliyotokea hivi karibuni na kuzihimiza mamlaka na wananchi kuzingatia misingi ya haki na amani iliyopo nchini.

"Katika kipindi cha mwezi mmoja na nusu, Tume imekuwa ikifuatilia kwa karibu matukio ambayo yanajitokeza nchini na baada ya kufanya tathmini kuhusu matukio hayo tumejiridhisha kuwa yanaashiria uvunjifu wa haki za binadamu, ukiukwaji wa misingi ya utawala bora na uvunjifu wa amani na utulivu nchini", alisema Jaji Mstafu Mwaimu.

Aliongeza kuwa katika kipindi cha kuelekea uchaguzi mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani, kumekuwa na matukio mbali mbali yakiwemo matumizi ya lugha chafu zisizozingatia utu na heshima ya mtu zinazoleta hamasa na kuchochea uvunjifu wa amani na utulivu.

Alieleza kuwa pamoja na hayo pia tume imebaini kuwepo kwa matukio yanayoashiria matumizi ya nguvu kupita kiasi wakati wa kushughulikia mikusanyiko ya kisiasa, kushambuliwa na kujeruhiwa kwa baadhi ya wananchi.

Aidha Jaji Mwaimu alisema THBUB inalitaka Jeshi la Polisi liendelee kuwasaka na kuwachukulia hatua za kisheria watu waliohusika na kujeruhiwa kwa Dk. Kitima, waliomteka 'Mdude' na waliohusika katika matukio mengine ya uvunjwaji wa haki za binadamu.

"THBUB inalaani matukio hayo na inaona kuwa vitendo vinavyojitokeza havitoi taswira nzuri katika ustawi wa haki za binadamu, utawala bora na amani na utulivu nchini ambayo ni muhimu sana katika kipindi hiki tunapoelekea katika uchaguzi mkuu", alisema.

Alifafanua kuwa THBUB inatambua kuwa kwa mujibu wa katiba, sheria za nchi na mikataba mbali mbali ya kimataifa ya haki za binadamu ambayo Tanzania imeridhia, wananchi wote wanayo haki ya kufurahia na kupata haki zao za binadamu hivyo kila mmoja achukue jukumu la kuziheshimu na kuzilinda.

# Uturuki, Zanzibar

**NA ASIA MWALIM**

MBUNGE wa Jimbo la Fuoni, Abasi Ali Mwinyi, amesema mashirikiano kati ya Serikali ya Uturuki na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yanasaidia nchi kupata nyenzo muhimu na fursa za kukuza uchumi endelevu.

Aliyasema hayo alipokuwa akifunga mafunzo ya siku tano kwa watendaji wa Ofisi ya Nyaraka na Kumbukumbu Zanzibar yaliyotolewa na Taasisi ya Uratibu wa Maendeleo ya Uturuki - Tanzania (TIKA), katika ofisi za Nyaraka Kilimani mjini Unguja.

Alisema ubora huo unatokana na misaada ya elimu na ujuzi wanaotoa Uturuki kwa wananchi wa Zanzibar ambao utaifanya Zanzibar kujitegemea hasa katika masuala ya sayansi na teknelojia.

Aidha alisema licha ya mafunzo, Uturuki imekua ikitoa msaada mkubwa Zanzibar kwa kuziunga mkono sekta tofauti ikiwemo afya na miundo mbinu ya barabara.

